Teacher.co.ke

# MTIHANI WA KANDA YA BUKAKA

**102/2 KISWAHILI MACHI,2025**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**KIDATO CHA NNE**

1. **UFAHAMU** **(ALAMA 15)**

a) Eleza jinsi dhuluma dhidi ya watoto inavyojitokeza katika kifungu ulichosoma. (alama 2)

I. **Watoto kuajiriwa kama vijakazi, vibarua, kuchunga mifugo, kutafuta kuni**
II. **Watoto kufanyiwa ukatili/ kufanyishwa kazi za ukahaba**

b) Bainisha maudhui manne ambayo Bw.Bonaya Kase anadokeza katika mazungumzo yake. (alama 4)

I. **Umaskini**
II. **Ajira ya watoto**
III. **Biashara haramu**
IV. **Mimba za mapema**
V. **Haki za watoto**

c) Tambua suluhisho kwa matatizo yanayowakumba watoto kwa mujibu wa kifungu. (alama 2)

I. **Kubuni rasimu ya sera ya kuwalinda watoto**
II. **Kuwepo kwa taasisi maalumu ya kufuatilia maslahi ya watoto**

d) Nchi inahatarishwa ikiwa hatua za dharura hazitachukuliwa kukabiliana na ulanguzi wa watoto. Taja washikadau wanaoweza kushirikishwa ili kumaliza tatizo hili. (alama 2)

**i. Polisi**

**ii. Afisi ya mkurugenzi mkuu wa mashtaka ya umma**

**iii. Maafisa wa Idara ya Mahakama**

**iv. Maafisa wa idara ya uhamaji**

e) Kipe kifungu hiki anwani mwafaka. (alama 1)
**Ukiukaji wa haki za watoto/Haki za watoto**

f) Eleza mchango wa wazazi katika kukiuka haki za watoto. (alama 2)
**Wazazi hutumia watoto kama wafanyakazi**
**Wazazi hutelekeza jukumu la malezi. Hivyo wanafunzi wengi huacha shule**

g) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika kifungu. (alama 2)

**i.** kitovu – **chanzo/asili**
ii. ulanguzi – **uhamisho wa watoto kwa lengo la kuwatumia vibaya**

***Tanbihi:***
***{Adhibu hadi makosa yote ya sarufi yanapojitokeza kwa mara ya kwanza ila adhabu isizidi alama alizotuzwa mtahiniwa katika sehemu/kisehemu.Aidhaa,adhibu hadi makosa 6 ya hijai yanapojitokeza kwa mara ya kwanza.}***



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

**2. UFUPISHO** **(ALAMA 15)**

a) Fupisha ujumbe wa aya tatu za kwanza kwa maneno 55. (alama 6, 1 mtiririko)

i. Kenya ilikuwa koloni ya Uingereza.
ii. Nchi ilishuhudia mapambano ya uhuru ili kuikomboa
iii. Wengi waliohusika walikuwa wanaume.
iv. Wanawake walichukuliwa kama wasio na umuhimu kiuchumi na mamlaka.
v. Hata hivyo baadhi ya wanawake walisimama kidete na kujukumika katika safari ya uhuru wa Kenya.
vi. Wengine walitunga na kuimba nyimbo zilizokejeli serikali ya kikoloni.
vii. Wengine walikuwa majasusi wa wapiganiaji uhuru wa Mau Mau.

*(hoja zozote tano, ut 1)*

b) Tambua mchango wa wanawake mahsusi katika mapambano ya ukombozi. (maneno 105-110). (alama 9, 1 mtiririko)

i. Mekatalili wa Menza alipinga utawala wa kikoloni wa Uingereza Pwani.
ii. Aliongoza Wagiriama kuasi Waingereza waliotishia uhuru wao kupitia kazi za kulazimishwa na kutozwa ushuru.
iii. Muthoni Kiriima alikuwa mpiganaji wa ngazi ya juu ya Mau Mau.
iv. Muthoni alisaidia kuwapa wapiganaji chakula na maji na kufanya kazi kama jasusi.
v. Alikuwa na cheo cha jenerali kisha akawa *Field Marshal*
vi. Alikabiliana na hali mba ya msituni.
vii. Wambui Otieno aliwafanyia Mau Mau kazi ya upelelezi jijini Nairobi
viii. Alikuwa mwanaharakati na mpiganaji
ix. Alihudumu kwa kupeleleza, kuwasiliana na kusaidia katika ununuzi wa silaha.
x. Alijihusisha na shughuli za vyama vya wafanyakazi.
xi. Alihamasisha wanawake kugoma na kufanya ghasia dhidi ya utawala wa Waingereza.
xii. Mukami Kimathi alishiriki kikamilifu katika harakati za kupigania uhuru wa nchi.
xiii. Mukami alizuiliwa jela la Kamiti wakati wa harakati za kupigania uhuru.
xiv. Alimuunga mkono mumewe alipokuwa kiongozi wa Mau Mau.

*(Hoja zozote nane ut 1)*

***Tanbihi;***

*{**Adhibu hadi makosa 6 ya sarufi na 6 ya hijai pindi yatokeapo kwa mara ya kwanza**}*

**3. MATUMIZI YA LUGHA** **(ALAMA 40)**

**a) chura 1/0**

b) matumizi ya -li-



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

Tunda lilipatikana sokoni.
**li-ngeli ya LI-YA**
**li-wakati uliopita** **1x2=2**

c) **Mara kwa mara – kielezi cha idadi/kiasi/idadi jumla**
**Shambani- kielezi cha mahali** ***kutaja ½ kuainisha ½*** **½ x4=2**

d) Miundo ya nomino katika ngeli ya U-ZI huku ukitoa mifano.
**u-mb-ubao-mbao**
**u-ny-uzi-nyuzi**
**u- ~~ø~~-uteo – teo**
**w-ny-wembe-nyembe**
**u-nd-udevu-ndevu/ulimi-ndimi** **(2x1=2)**

e)
i. **Gari lililonunuliwa baba na bintiye limemfanya afurahi. (2/0)**
ii. **Kipkeino alikimbia mbio leo/jana/juzi/jioni/asubuhi. (2/0)** ***kadiria***
iii. **Mwalimu mzuri alituzwa.** **(2/0)**

f) Tambua aina ya vishazi katika sentensi ifuatayo.
Ajaye shuleni ni mzazi wake.
**Ajaye shuleni – kishazi tegemezi**
**Ni mzazi wake - kishazi huru**
**Kutambua ½ kuainisha ½** **(½ x4=2)**

g) Andika katika udogo.
Vitabu vilivyokuwa vimebebwa na mwanamke vimeuzwa.
**Vijitabu vilivyokuwa vimebebwa na kijanajike vimeuzwa.** **(2/0)**

h) Matumizi mawili ya mkwaju.
**Mvyele/mzazi atahitajika.** **-Kuonyesha maneno yenye maana sawa/visawe**
**Kijana alizaliwa tarehe 1/1/2022.** **Hutumika kuandika tarehe** **(1x2=2)**

i) Andika katika usemi halisi.
Mama alimuamrisha mtoto alale.
**"Kalale!" Mama alimuamrisha mtoto.**
**"Lala!" Mama alimuamrisha mtoto.**
**"Nenda ukalale!" Mama alimuamrisha mtoto.** **(½ x6=3)**

j) Tungasentensiukitumiamzizi **-ch-**katikakauliyakutendea.

**Asubuhi njema ilimchia banati huyo.(pambazuka)** **1/0**

**Au**

**Waimbaji walimchia Mungu kupitia nyimbo zao.(ogopa)**

k) Tambua hali iliyotumika katika sentensi ifuatayo.
Kidege chapaa angani.
**Hali ya 'a' isiyodhirika** **1/0**



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

l) Ainisha virai katika sentensi ifuatayo.
Jumba hili limejengwa vyema na fundi hodari mno
**Kirai nomino/RN – Jumba hili/Fundi hodari mno/jumba/fundi**
**Kirai tenzi/RT-limejengwa vyema**
**Kirai husishi/RH – na fundi**
**Kirai vumishi/ RV – hodari mno** **(½ x4=2) zozotembili**

m) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha mishale.
Wale walifika mapema lakini hawa wangu walichelewa. (al 4)
S → S1+U+S2
S1 → KN+KT
KN → W
W → Wale **alama 2**
KT → T+E
T → walifika
E → mapema
U → lakini
S2 → KN+KT
KN → W+V
W → hawa
V → wangu **alama 2**
KT → T
T → walichelewa

n) Unda nomino kutokana na kitenzi: tubu.
**toba/kutubu/mtubia/kitubio.1/0**

o) Bainisha maana tatu katika sentensi inayofuata.
Mandila aliwatangazia chao

I. **Utata ukikitwa kwenye tangazia-kwa niaba yao/kwa sababu/alitumia wao kama kifaa cha kutangaza.**
II. **Utata ukikitwa kwa chao-kifaa cha kutenda jambo/cha Mandila na wengine/wengine ambao hawapo.**
III. **Ukikitwa kwa shamirisho wa katika aliwatangazia-watu wengine(wao)/ nyinyi(nafsi ya pili)** **(maana zozote 3x1=3)**

p) Tunga sentensi ukitumia kuhusisishi cha mtenda.
**Mtoto amenunuliwa maziwa na mama. Kadiria sentensi zilizo na (na) (1/0)**

q) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo.
Mwizi alikimbia haraka aliposahau njia.
**Mwizi alitembea polepole alipokumbuka njia.** **(1/0=1)**
**{Vinyume hutolewa kwa vitenzi,vivumishi,vielezi na vihusishi pekee.Hakuna kinyume cha nomino}**

r) Andika neno lenye mofimu zifuatazo.
Kikanushi, ngeli(KI-VI umoja), wakati kanushi uliopita, mzizi, kauli ya kutendeka, hali ya kutenda.
**Hakikupigika/hakikulika/ Hakikulimika/Hakikusomeka-kadiria(½ x6=3)**

s) Amrisha katika nafsi ya tatu wingi.
**Waamke!** **(1/0)**


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

t) **Kiambaza/uzio/ua**
**vurugu/zogo/vurumai/fujo/ghasia (1x2=2)**

***Tanbihi***

***{Adhibu makosa yoyote ya sarufi yanapojitokeza kwa mara ya kwanza ila idadi ya makosa ya sarufi isizidi alama zilizotuzwa mtahiniwa katika sehemu au kisehemu. Aidha,adhibu hadi makosa 6 ya hijai pindi yatokeapo kwa mara ya kwanza}***

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

**4. ISIMUJAMII (ALAMA 10)**

a) Sajili ya bungeni (1/0)

b) Sifa ya sajili ya bungeni

i. Lugha hunukuu vifungu kutoka kwa katiba ya taifa.
ii. Huwa na sentensi ndefu kuliko kawaida
iii. Lugha huwa sanifu ili kuzuia utata kutokea
iv. Lugha ya adabu/heshima hutumika-Bw.Spika
v. Huwa na msamiati maalumu- spika, mswada
vi. Kuna kuchanganya na kubadilisha msimbo-
vii. Lugha ina sifa ya unyenyekevu pamoja na kutaja nyadhifa za watu. Mfano, Mheshimiwa,Mtukufu rais.
viii. Lugha huwa na uradidi mwingi. Mfano. Bwana spika
ix. Kuna sifa ya kukatizana usemi. Hasa anayezungumza anapopotoka.
x. Hutumia mtindo maalumu wa kuanzisha, kuendeleza na kutamatisha mazungumzo
xi. Kuna matumizi ya ishara. Mfano, wajumbe kuinama kwa heshima ya spika wanapoingia na kutoka. (zozote5 1x5=5)

***Kadiria mifano ya mwanafunzi***

{**Tanbihi kila sifa lazima ifafanuliwe kwa kutolewa mfano ndiposa apate alama kamili.Sifa bila mfano ni nusu alama}**

c) Jadili changamoto nne zinazokumba kuimarika kwa Kiswahili katika jamii ya sasa. (alama 4)

I. Matumizi kiholela ya lugha bila kuzingatia kanuni za kisarufi miongoni mwa wananchi.
II. Athari za lugha nyingine za kiafrika
III. Athari za sheng' miongoni mwa vijana
IV. Uhaba wa machapisho kwa lugha ya Kiswahili
V. Somo la Kiswahili kutengewa vipindi vichache shuleni ikilinganishwa na somo la Kiingereza.
VI. Masomo mengi shuleni hufunzwa kwa lugha ya Kiingereza kuanzia shule ya malezi isipokuwa somo la Kiswahili



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

VII. Matumizi mabaya ya Kiswahili kwenye vyombo vya habari ambavyo vinahitajika kukuza Kiswahili.

VIII. Kasumba ya kikoloni miongoni mwa wananchi kuwa Kiswahili ni lugha ya hadhi ya chini inayotumika na wasiosoma.

*IX.* Kutokuwa na sera madhubuti inayoelekeza kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili .***(hoja zozote nne zilizofafanuliwa kikamilifu 1x4=4)***

***{Adhibu hadi makosa 4 ya sarufi na 4 ya hijai yanapojitokeza kwa mara ya kwanza}***

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes